**PATANDI MAALUM SECONDARY SCHOOL**

**P.O BOX 173, ARUSHA.**

**Mobile No. +255 764751066**

**FOMU NA…………..** **TAREHE……………………………**

**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2026 KATIKA SHULE YA SEKONDARI PATANDI MAALUM ILIYOPO WILAYA YA ARUMERU MKOA WA ARUSHA**

## 1) UTANGULIZI

Shule hii ni ya **SEKONDARI YA KUTWA NA BWENI MCHANGANYIKO** (wavulana na Wasichana). Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha KWANZA mwaka wa masomo 2026. Shule itafunguliwa tarehe **13/01/2026**. Mwanafunzi afike na vifaa vyote alivyoagizwa na kwa muda uliotajwa hapo juu.

## 2) MAHALI SHULE ILIPO

Shule ipo mkoa wa Arusha wilaya ya Arumeru katika Halmashauri ya Meru. Shule ipo umbali wa kilomita 11.5 kutoka Arusha mjini na kilomita 8 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Meru kutokea Moshi kuelekea Arusha. Shuka kituo cha mabasi cha Tengeru na kuelekea shuleni ambayo ipo ndani ya Chuo cha Ualimu Patandi (Mita 200 kutoka stendi ya Tengeru).

Yafuatayo ni maelezo na maagizo ambayo unashauriwa kuyatumia kabla hujafika hapa shuleni

## 3) AFYA

Mwanafunzi apimwe na Daktari aliye na dhamana ya kutoa huduma hiyo kwa kujaza fomu iliyoambatanishwa. Ni vyema mzazi au mlezi awe wazi juu ya afya ya mtoto wake kwani kuficha tatizo la afya inaweza kuhatarisha maisha ya mtoto.

Mwanafunzi aje na kadi ya bima ya afya kama atakuwa nayo kwa ajili ya kurahisisha gharama za matibabu.

## 4) TAALUMA

Mwanafunzi atawajibika kufanya mazoezi na mitihani yote bila kukosa kwa wakati uliopangwa.

Ni wajibu wa mzazi kupata au kudai ripoti ya maendeleo ya mtoto wake kila baada ya muhula wa masomo. Kila Mwanafunzi anapaswa kuweka juhudi katika Masomo.

Lugha inayotumika katika mawasiliano ni **KIINGEREZA na LUGHA YA ALAMA** nje na ndani ya darasa isipokuwa wakati wa somo la Kiswahili tu

## 5) USAFI.

i. Kila Mwanafunzi anatakiwa kuonekana nadhifu nje na ndani ya darasa kimwili na kimavazi wakati wote, nywele ziwe fupi na zichanwe vizuri.
ii. Mwanafunzi atawajibika kuvaa sare ya shule muda wote isipokuwa wakati wa michezo na kazi za nje.
iii. Kila mwanafunzi atawajibika kutunza:
    - Vifaa vyake binafsi mfano: mavazi, daftari na vifaa vingine vyovyote vya shule atakavyokabidhiwa.
    - Mahali atakapolala patandikwe vizuri na vifaa binafsi vipangwe kwa unadhifu.
    - Kutunza mazingira ya nje na ndani ya darasa na bweni. Ni marufuku mwanafunzi kutupa taka au karatasi ovyo ndani ya darasa au katika mazingira ya shule.
iv. Mwanafunzi atakayeharibu kifaa chochote cha shule au cha mwenzake atalazimika kulipa (Mzazi wake atalazimika kulipa na akishindwa kulipa atafukuzwa shule). Kila mwanafunzi atatakiwa kutunza kuta na sakafu ya Madarasa, Mabweni, Bwalo la kulia chakula, Maktaba, Maabara pamoja na vifaa vingine vilivyoko katika eneo la shule,
v. Mwanafunzi yeyote hataruhusiwa kuingia na chakula cha aina yeyote bwenini.

## 6) WAGENI

i. Wazazi wanapofika shuleni kwa jambo lolote, Mzazi aonane na Mwalimu wa zamu au Mkuu wa shule kupata kibali cha kuonana na mwanafunzi.
ii. Ni marufuku mwanafunzi kupokea au kuletewa chakula kutoka nje ya shule na mzazi,ndugu, jamaa, au kununua kwa wale wanaotembeza njiani.
iii. Ni marufuku kwa mzazi/mlezi yeyote kumletea mwanafunzi chakula au kinywaji cha aina yeyote pindi atakapomtembelea.

## 7) SARE YA SHULE

### I. WAVULANA

i. Suruali 2 za rangi ya **Dark blue** (chini ziwe na inchi 16-18 kutokana na urefu wa mwanafunzi na iwe na mkunjo.
ii. Shati 2 za tomato nyeupe za mikono mifupi.
iii. Sweta ya rangi dark blue sawa na rangi ya suruali.
iv. Tai rangi ya dark blue yenye mistari meupe
v. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba na visiwe na visigino virefu.
vi. Soksi dark blue/nyeusi jozi 2 au Zaidi,
vii. T - Shirt mbili ya rangi kijivu yenye kola
viii. Mkanda mweusi usio na urembo pamoja na bukta.
ix. Suruali nyeusi 2 kwa ajili ya shamba dress na shati mbili za draft ndogo rangi nyeusi na nyeupe
x. Nguo za Michezo (nguo za michezo iwe ya NYEKUNDU Tshirt na bukta nyekundu) , viatu vya michezo nyeusi(raba) .
xi. Tracksuit ya rangi KIJIVU kwa wanafunzi wote.
xii. Pullneck nyeusi kwa ajili ya kuvaa ndani ya shati la shule wakati wa baridi.
xiii. Saa ya mkononi kwa ajili ya kutunza muda ila isiwe na kikokotozi (calculator)
xiv. Sahani na kikombe cha bati pamoja na kijiko.
xv. File za kuhifadhia kumbukumbu za wanafuzi.

**II. WASICHANA**

i. Sketi 2 zenye draft ziwe na rinda box mbili kubwa mbele na nyuma na rinda 6 mbele na nyuma urefu chini ya goti.
ii. Shati 2 za tomato nyeupe za mikono mifupi.
iii. Sweta rangi dark blue.
iv. Hijabu nyeupe isiyo na urembo wowote kwa wasichana waislam watakaopenda kuvaa
v. Tai rangi ya darkblue iliyokolea,T-shirt rangi nyeupe yenye kola isiyo na maandishi yoyote,
vi. Gauni la draft darkblue na nyeupe kwa ajili shamba dress.
vii. Tracksuit rangi ya KIJIVU (kwa wanafunzi wote).
viii. Soksi za rangi nyeupe ndefu mpaka juu ya goti stoking pea 2, viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba visiwe na visigino virefu.
ix. Raba za michezo rangi nyeupe
x. Nguo za Michezo (iwe ya **NYEKUNDU** Tshirt na bukta yake).
xi. Pullneck nyeusi kwa ajili ya kuvaa ndani ya shati la shule wakati wa baridi.
xii. Sahani na kikombe cha bati pamoja na kijiko.
xiii. File za kuhifadhia kumbukumbu za wanafuzi.
xiv. Saa ya mkononi kwa ajili ya kutunza muda ila isiwe na kikokotozi (calculator)

**<u>NB:</u>**

Sample ya kitambaa cha sare ya shule na shamba dress vimeambatanishwa kwenye fomu ya kujiunga na shule. (kwa wanafunzi wa mikoani ambao watakosa kitambaa vinapatikana Arusha).

**8) <u>MAHITAJI MENGINE MUHIMU KWA WANAFUNZI WA BWENI</u>**

i. Sanduku la bati dogo la kuwekea vifaa vyake (trunker), kufuli na begi dogo la kusafiria.
ii. Arusha ni sehemu ya baridi, mwanafunzi aje na blanketi moja zito, shuka 2 za rangi ya light blue(Kwa wavulana), foronya 2 za rangi ya light blue kwa wavulana na shuka 2 ya rangi ya pink pamoja na foronya zake kwa wasichana, mto pamoja na neti nyeupe.
iii. Aje na tochi(sio ya kuchagi kwa umeme), mswaki na dawa ya meno, sabuni za kufulia na kuogea pamoja na taulo.
iv. Ndoo 2 ndogo za plastiki
v. Aje na toilet paper kwa ajili ya matumizi yake binafsi.
vi. Mpatie mwanao hela ya matumizi binafsi ikiwemo ya dharura na matibabu.
vii. Mfungulie mwanao akaunti benki kwa ajili ya fedha ya matumizi .hairuhusiwi kutuma fedha kwa mwanao kupitia kwa walimu.
viii. Nauli ya kurudia nyumbani wakati wa likizo. Haturuhusu mwanafunzi kubaki shuleni wakati wa likizo.

**NB.Kwa wazazi wenye Watoto wenye mahitaji maalum ambao wanahitaji usaidizi wa walezi watoe taarifa kwa uongozi wa shule mara mzazi atakapopata taarifa ya mtoto kupangwa Patandi.**

## 9. VIFAA VINGINE

i. Madaftari (12) kumi na mbili quire 3 au zaidi.
ii. Mathematical set (Mkebe wa Hesabu)
iii. Begi la shule la kuhifadhia madaftari na vitabu, isiwe mfuko wa rambo, malboro, adidas au mfuko wa salfet.
iv. Kalamu nyeusi au blue (zisiwe kalamu za rangi nyekundu), penseli za kutosha, ruler sm 30 na kifutio.
v. Madaftari 12 saizi ya kati yasiwe madogo sana kwa ajili ya mazoezi ya kila siku kwa kila somo.
vi. Kila mmoja aje na fagio ngumu (hard broom) 1, squeezer 1, fyekeo 1, jembe na mpini.
vii. Kila mmoja aje fagio wa chelewa uliojaa vizuri.
viii. Cheti cha kuzaliwa.
ix. Rimu 1 (Karatasi nyeupe)

## 10. SHERIA ZA SHULE YA SEKONDARI PATANDI MAALUM

i. Kila mwanafunzi atawajibika kutii sheria, kufuata ratiba na kufuata taratibu zote za shule zinazotolewa na uongozi mzima wa shule kwa mfano; Mkuu wa shule , Msaidizi wa Mkuu wa shule, Walimu, Viongozi wa baraza la wanafunzi na wahudumu wengine wote.
ii. Kila mwanafunzi atawajibika kuwa na mwenendo wa heshima na adabu njema kwa watu wote, wakubwa kwa wadogo, viongozi na wenzake.
iii. Kila mwanafunzi aonyeshe nidhamu katika kuvaa sare ya shule ndani au nje ya mipaka ya shule kwa muda uliowekwa na uongozi wa shule.
iv. Kila mara mwanafunzi awe na nywele fupi za saizi moja, ni marufuku kunyoa mitindo ya aina yoyote na kucha ziwe fupi.
v. Kila Mwanafunzi atalazimika kutii kengele, kuwahi darasani, michezoni, bwaloni na mahali popote atakapohitajika. Daima Mwanafunzi ajaribu kuonekana mkakamavu na mwenye mahusiano mazuri na wenzake na jumuiya nzima ya shule.
vi. Mwanafunzi atawajibika kula chakula kitakachoandaliwa na shule ndani ya bwalo na kwa wakati unaotakiwa. Pia atatakiwa kuosha na kutunza chombo chake cha kulia chakula/kunywa maji n.k.
vii. Mwanafunzi haruhusiwi kwenda na chakula cha aina yeyote Bwenini.
viii. Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kuja na aina yoyote ya chakula au kinywaji pindi arudipo shuleni kutoka nyumbani wakati wa likizo.

## 11. MAKOSA YA KUJIFUKUZISHA SHULE MOJA KWA MOJA

i. Wizi au unyang`anyi wa aina yeyote ndani au nje ya shule.
ii. Utoro wa shule wa muda mrefu (siku 90 bila taarifa).
iii. Utovu wa nidhamu unaosababishwa na matendo ya zinaa, uasherati, unajisi, kulawiti, kubaka au unyanyasaji wa kijinsia.
iv. Kudanganya katika mitihani au mazoezi, kwa maandishi au kuchungulia kwa mwenzake darasani.
v. Utumiaji wa pombe aina yeyote, uvutaji wa sigara, bangi, mirungi na utumiaji wa madawa ya kulevya.
vi. Kushiriki, kushawishi au kuanzisha mgomo shuleni.
vii. Utumiaji wa lugha za matusi au kebehi kwa kusema au kuandika au kuchora ukutani, ubaoni, sakafuni na hata kwenye siling board kuhusu uongozi wa shule, walimu, wanafunzi wenzake au wahudumu wengine wa shule.

viii. Kukataa kufuata ratiba ya shule au kutotii sheria za shule.
ix. Kumiliki na kutumia simu yake au simu inayomilikiwa na mwanafunzi mwingine akiwa shuleni, au kuwa na laini ya simu.
x. Ukaidi, kiburi, kugomea adhabu kwa makusudi na kusema uongo.
xi. Kujenga urafiki wa kimapenzi baina ya mwanafunzi wa jinsia yeyote, nje au ndani ya shule.
xii. Kupata mimba, kutoa mimba au kusababisha mimba kwa mwanafunzi.
xiii. Kuoa au kuolewa.
xiv. Kutoa lugha chafu ya matusi kwa wanafunzi, walimu na watumishi wengine.
xv. Kupiga au kupigana na mwanafunzi, mwalimu au mfanyakazi yeyote.

Kwa niaba ya uongozi wa shule ya Sekondari ya Patandi Maalum napenda kuwakaribisha sana katika jumuiya hii.

**NB**.Kwa mwanafunzi wenye changamoto za kiafya mzazi/mlezi hakikisha unaonana na uongozi wa shule ili uweze kuelezea changamoto za mtoto ili aweze kupewa huduma stahiki.

Pia uongozi wa shule unaomba wazazi/walezi waandike namba za uongozi wa kijiji wanakotoka watoto/wanafunzi.

Wako katika malezi ya vijana.

..............................................

Mwl. Janeth Mollel

**MKUU WA SHULE**

PATANDI MAALUM SEC SCHOOL
HEAD OF SCHOOL
DATE..................
SIGN..................
P.O.BOX

**FOMU YA AHADI**

Iwapo umezisoma sheria hizi na kuzielewa vyema na unakubali kuzifuata jaza fomu ifuatayo:

Mimi………………………………………………………………………………. (Jina la Mzazi/Mlezi)

Mzazi/Mlezi wa ………………………………………………………………… (Jina la Mwanafunzi) nimesoma masharti yote ya shule nimeyaelewa na kukubaliana nayo na ninaahidi mimi na mwanangu tutayafuata ipasavyo.

Sheria hizi ni mkataba kati yangu mimi mwanafunzi,uongozi wa shule na mzazi wangu.

…………………… ……………………………

SAHIHI YA MZAZI/MLEZI TAREHE

Mimi……………………………………………………………………………… (Mwanafunzi), nimesoma masharti yote ya shule na kuyaelewa na naahidi kuyatekeleza ipasavyo.

………………………. ………………………………

SAHIHI YA MWANAFUNZI TAREHE

Sahihi na Mhuri wa Mkuu wa shule

……………………………………………………….

(Fomu hii irudishwe siku ya kufungua shule baada ya kukamilika kujazwa)

## SHULE YA SEKONDARI PATANDI MAALUM

## FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULENI

**SEHEMU A: HABARI ZA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili (Kama kwenye mtihani) ……………………………………………………………………………
2. Tarehe ya kuzaliwa …………………………Dini…………………………Dhehebu……………………….
3. Mahali na wilaya ulipozaliwa………………………………………………………………………………
4. Shule ulipomaliza darasa la saba………………………………Mwaka uliomaliza………………………
5. Kidato unachokuja kuingia hapa Patandi Maalum Sekondari………………………………………………...
6. Namba yako ya mtihani wa darasa la saba………………………………………………………………………
7. Ifuatayo ni chati ya Uongozi wa kijiji/mtaa mtoto anapotoka

| NA. | JINA LA KIONGOZI | CHEO | MAHALI | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4 | | | | |

8. Kazi yoyote ya uongozi uliyowahi kufanya kama vile Kiongozi wa Michezo, Kwaya, Ngoma, Kiranja, Maktaba, n.k.

| NA | MADARAKA AU UONGOZI | SHULE/ MAHALI | MWAKA |
|---|---|---|---|
| 1. | | | |
| 2. | | | |
| 3. | | | |
| 4. | | | |
| 5. | | | |

9. Mambo unayopendelea kufanya nje ya masomo (kama vile mpira wa miguu, bustani, ushonaji wa viatu, nguo, michezo ya kuigiza, kuimba, n.k)
10. Ndugu wa karibu wa mwanafunzi (wa kiume/ wa kike) kama Mjomba, Mama, shangazi, Kaka, Dada, kufuatana na umri wao wa kuzaliwa:-

| NA. | JINA LA NDUGU | KAZI ANAYOFANY | UHUSIANO NA MWANAFUNZI | KIWANGO CHA ELIMU | ANUANI | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | | |
| 2. | | | | | | |
| 3. | | | | | | |
| 4. | | | | | | |

Nathibitisha kwamba habari zilizotolewa hapo juu ni za kweli. Naahidi kuwa na tabia nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo.

Sahihi ya Mwanafunzi……………………………………...… Tarehe ………………………………………

**SEHEMU A: HABARI ZA MZAZI/ MLEZI**

(Fomu hii ijazwe na Mzazi /Mlezi)

1) Jina kamili la Baba Mzazi/Mlezi…………………………………………………………………..
2) Kazi yake…………………………………Ofisi/Mahali anapofanyia kazi……………………………..
3) Mahali anapoishi……..…………………………………………………………………………….
   Anwani ya nyumbani..………………………………………………………………………………
   Kijiji………………………………...………… Kata……………………………….
   Tarafa………………………………..Wilaya………………………Mkoa…………………………
   Namba ya simu……………
4) Dini ya BabaMzazi/Mlezi……………………………Dhehebu…………………………………
5) Baba mzazi yupo hai/ amefariki (kata isiyohusika)

6) Jina kamili la Mama Mzazi/ Mlezi…………………………………………………………………..
7) Kazi yake…………………………………Ofisi/Mahali anapofanyia kazi……………………………
8) Mahali anapoishi ……………………………………………………………………………..
   Anwani ya nyumbani..………………………………………………………………………………
   Kijiji………………………………...………… Kata……………………………….
   Tarafa………………………………..Wilaya………………………Mkoa…………………………
   Namba ya simu………………………………………………………………………………………
   Dini ya Mama Mzazi/Mlezi……………………… Dhehebu………………………………………..
9) Mama mzazi yupo hai/ amefariki (kata isiyohusika)
9) Mtoto anaishi na *(Weka tiki* V)

(1) Baba tu ☐

(2) Mama tu ☐

(3) Wazazi wote ☐

(4)Mlezi /Walezi tu ☐

Mimi…………………………………………………………………………………………………..
..………………………………………

Mzazi/Mlezi wa……………………………………………………………………………..…………
nathibitisha kuwa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi. Naahidi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba mwanangu anakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii. Aidha nitakapohitajika shuleni wakati wowote nitafika kusikiliza wito.

Saini ya Mzazi/Mlezi………… Tarehe ……………..….. Namba ya simu…………………………

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MERU DISTRICT COUNCIL**
**PATANDI MAALUM SECONDARY SCHOOL**
**P. O. BOX 173, DULUTI – ARUSHA**
**SPECIAL REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

The Medical Officer
…………………………..
(GOVERNMENT M.O)

From Headmistress,
Patandi Maalum Secondary School
Date ………………………………

Name of Students…………………………..Date………………..Term……………………..Year……………
I shall be very grateful if you will kindly examine the above named student and give us a report regarding his fitness to undertake studies well in our school.

**A: PRELIMINARY INFORMATION: MEDICAL HISTORY**

| NO | DISEASE | YES | NO | | DISEASE | YES | NO | | DISEASE | YES | NO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Tuberculosis | | | 7 | Kidney/trouble | | | 13 | Operation | | |
| 2 | Asthma | | | 8 | Diabetes | | | 14 | Eye disorder | | |
| 3 | Pneumonia | | | 9 | Nervous breakdown | | | 15 | V.D | | |
| 4 | Heart Trouble | | | 10 | Ear/ Noise/ throat trouble | | | 16 | disabled | | |
| 5 | Recurrent indigestion | | | 11 | Skin disorder disease | | | 17 | | | |
| 6 | Jaundice | | | 12 | Anemia | | | 18 | | | |

**B. VITAL STATISTICS**
Age……………………Height……………………Weight……………………..Blood group…………..Blood Pressure……………………..Pulse rate……………..systolic……………….Diastolic……………………………….

**C. MEDICAL EXAMINATION**

| | **REMARKS/TREATMENT** |
|---|---|
| EAR | RT. LT………………….. |
| VISSION | RT. EYE LT. EYE |
| THROAT | |
| CHEST EXAMINATION | |
| ABDOMINAL EXAM | LIVER SPLEEN |
| | OTHER COMENTS |
| M.S SYSTEM | UPPER LIMBS |
| | LOWER LIMBS |
| ANY OTHER FINDING | |

**D. LABORATORY EXAMINATION/ INVESTIGATION**

1. STOOL- Ova…………………………. leucocytes…………………………………………………
2. URINALYSIS: PROTEIN……………………………………………………………………………
GLUCOSE…………………………………………………………………...
SEDMENT: - OVA……………………..Leucocytes…………………………………….
3. Hb……………………………………………………………………………………………………..

4. B/S…………………………………………………………………………………………………….
5. VDRL……………………………………………………………………………………………………
6. WBC Total………………………………………………………………………………………
   Differential: N……………L…………..M……….….E……………B………………..……
7. X- ray Chest (if necessary) ………………………………………………………………………………
8. ANY OTHER INVESTIGATION…………………………………………………………………………

**E. MEDICAL CERTIFICATION**

We request the medical officer to complete the following:

I have examined the above-named student and considered that he is physically fit/ unfit for most activities taken at the school as my findings indicated above.

Date…………….. Station…………………… Dr's Name…………………….. Signature……………………

Thank you in advance

**……………………………**
**JANETH MOLLEL**
**HEADMISTRESS**
**PATANDI MAALUM SECONDARY SCHOOL.**



Kitamba cha Suruali na sweta



Kitambaa cha Sketi wasichana



Kitambaa cha gauni la shamba dress na shati kwa wavulana